JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA HAMSINI NA SITA

24 JUNI, 2026

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA HAMSINI NA SITA – TAREHE 24 JUNI, 2026

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA FEDHA:

Maelezo ya Waziri wa Fedha kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2026 *(The Finance Bill, 2026)*.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2026 *(The Finance Bill, 2026)*.

III. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):

668. MHESHIMIWA THOMAS MAGANGA KAMPALA (KATAVI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanza ujenzi wa uzio na njia za kuunganishia majengo *(walkways)* katika Hospitali ya Halmashauri ya Mlele.

669. MHESHIMIWA SILVERY LUBOJA SALVATORY (MISUNGWI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Kituo cha Afya Lubili ili kusogeza huduma kwa Wananchi.

670. MHESHIMIWA FARAJI BURIANI NANDALA (NDANDA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itachukua hatua madhubuti dhidi ya uvamizi wa Jamii ya Wafugaji katika maeneo ya Wakulima wa ushoroba wa Mto Lukuledi - Ndanda.

OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):

671. MHESHIMIWA DKT. DAMAS DANIEL NDUMBARO (SONGEA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuendeleza eneo la TISEZA (EPZA) Mwengemshindo Songea.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

672. MHESHIMIWA DKT. REGINA CHRISTOPHER MALIMA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, lini Serikali itaanzisha Mafunzo ya Uvuvi wa Vizimba katika Chuo cha VETA Ukerewe ili kutoa ujuzi na ajira kwa Vijana wanaojihusisha na uvuvi.

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

673. MHESHIMIWA INNOCENT LUGHA BASHUNGWA (KARAGWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, lini Serikali itaanzisha ufugaji wa Samaki kwa Vizimba katika Maziwa ya Rugu, Lwakajunju na Kabuli ili kuongeza ajira na kipato.

WIZARA YA KILIMO:

674. MHESHIMIWA ABDALLAH DADI CHIKOTA (NANYAMBA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka vivutio kwa Wabanguaji Korosho wa ndani ili kuongeza kiwango cha Korosho kinachobanguliwa nchini.

675. MHESHIMIWA ENG. FADHILI SANDALI CHILOMBE (TUNDURU KUSINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itakamilisha Skimu za Umwagiliaji katika Vijiji vya Mkotamo, Naikula, Mbati, Misyaje na Nasya.

WIZARA YA UJENZI:

676. MHESHIMIWA ABUBAKAR DAMIAN ASENGA (KILOMBERO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya kutoka Ifakara - Ulanga, Ifakara - Malinyi na Ifakara - Mlimba.

677. MHESHIMIWA YUSTINA ARCADIUS RAHHI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Barabara ya Mbulu – Garbabi kwa kiwango cha lami.

IV. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima na Kusomwa Mara ya Tatu)

Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2026 *(The Finance Bill, 2026)*.

DODOMA
24 JUNI, 2026

BARAKA I. LEONARD
KATIBU WA BUNGE